TANGAZO LA SERIKALI Na. 135 la tarehe 21/2/2025

SHERIA YA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWENYE POMBE KALI YA ETHILI KWA MACHUGU INVESTMENT YA MWAKA 2025

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwenye Pombe Kali ya Ethili kwa Machugu Investment ya Mwaka 2025 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 19 Disemba, 2024.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3 na masharti mengine yoyote kama yatakavyoainishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, ushuru wa bidhaa unaopaswa kulipwa kwa bidhaa kwenye Pombe Kali ya Ethili iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii iliyoingizwa ndani au kununuliwa kabla ya kibali kupitia forodha kwa niaba ya au na Machugu Investment unasamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utakoma na ushuru wa bidhaa utapaswa kulipwa kana kwamba Amri hii haijatolewa ikiwa bidhaa tajwa itatumika kwa matumizi mengine au kuhamishwa au kuuzwa kwa mtu mwingine ambaye hastahili kupata manufaa yanayotolewa na Amri hii.

Ukomo

4. Amri hii itafika ukomo wake baada ya Machugu Investment kuondolewa wajibu wa kulipa kiasi cha ushuru wa bidhaa kwenye pombe kali ya ethili kwa kiasi cha shilingi bilioni moja na milioni mia nne.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| NA. | MAELEZO | KIPIMO | KIASI |
|---|---|---|---|
| 1. | Pombe Kali ya Ethili | Lita | 200,000 |

Dodoma,
18 Februari, 2025

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*